Tangazo la Serikali Na. 584 la tarehe 18-12-2015

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA YA 290

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) (z) na 16(1))

SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA ZA MWAKA, 2015

Jina na tarehe ya kuanza kutumika.

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Kodi ya Huduma**)** za Halmashauri ya Wilaya ya Geita za Mwaka, 2015 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Eneo la kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

Tafsiri.

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Muidhinishwa" maana yake ni mtumishi yeyote wa Halmashauri au mtu yeyote mwingine atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

"Hesabu" maana yake ni jumla ya mauzo au manunuzi ikiwa ni pamoja na kodi na ada katika mwaka husika wa mapato;

"Hesabu za mwisho" maana yake ni taarifa za kihasibu zinazowasilishwa na kampuni au taasisi yoyote ya kibiashara iliyosajiliwa baada ya kipindi cha hesabu kwa mujibu wa kifungu cha 9 cha Sheria Ndogo hizi,

zikijumuisha nyaraka, hesabu au maelezo yoyote yahusuyo kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizowasilishwa, zilizosambazwa, zilizotolewa na, au kuuzwa kibiashara.

"Kipindi cha hesabu" maana yake ni muda ambao mfanyabiashara, kampuni au taasisi ya kibiashara itatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara zake.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita au Afisa yeyote atakayeteuliwa kwa wakati huo kukaimu nafasi ya Mkurugenzi.

"Kamati za tathmini" ni kamati zinazoweza kuundwa na Halmashauri kama itakavyoona inafaa kwa ajili ya kufanya tathmini ya viwango vinavyopaswa kulipwa au vitakavyolipwa na mtu, watu au taasisi yoyote katika Sheria ndogo hii.

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa sura ya 290.

"Kodi ya huduma" maana yake ni malipo yanayotolewa kwa Halmashauri na mlipa kodi bila kujali mahali yalipo makao makuu ya mlipa kodi anayehusika.

"Wakala" maana yake ni mtu, kikundi cha watu au kampuni iliyoingia mkataba na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ushuru wa huduma.

Ukusanyaji wa Kodi ya Huduma

4.-(1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi Halmashauri itatoza na kukusanya kodi ya huduma kutoka kwa kila mfanyabiashara mwenye leseni, taasisi au kampuni yoyote ya kibiashara inayofanya shughuli zake katika eneo la mamlaka ya Halmashauri.

(2) Halmashauri itatoza na kukusanya kodi ya huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kutoka kwa mfanyabiashara mwenye leseni, taasisi au kampuni kila mwaka wa mapato kwa kiwango kisichozidi asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya hesabu za shughuli zote zikiwemo za uzalishaji wa bidhaa au utoaji huduma kutoka nje ya nchi zinazofanyika katika eneo la Halmashauri ukiondoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kodi ya mlaji.

Uwasilishaji wa taarifa zinazohusu shughuli za kibiashara

5. Mkurugenzi kwa taarifa ya maandishi, anaweza kumtaka mlipa kodi au wakala yeyote kuwasilisha hesabu zenye taarifa kamili za shughuli za kibiashara zikionyesha kiasi na thamani ya fedha ya bidhaa, au huduma zilizowasilishwa, kutolewa, kuingizwa, kusambazwa au kuuzwa kibiashara na taarifa ya fedha katika kipindi maalum kisichozidi siku thelathini tangu tarehe ya taarifa hiyo.

Uwasilishaji wa taarifa

6. Mtu yeyote ambaye atakuwa na taarifa kuhusu mfanyabiashara mwenye leseni, taasisi au kampuni ya kibiashara inayokwepa kulipa kodi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, atatakiwa kuwasilisha taarifa kuhusu jambo hilo kwa Mkurugenzi au Afisa Muidhinishwa.

Uwezo wa kuingia kwenye jengo au eneo

7. Mkurugenzi anaweza kumuagiza kwa maandishi Afisa Mwidhinishwa kuingia kwenye jengo au eneo la mlipa kodi au wakala kwa nia ya kufanya ukaguzi na tathmini ya kumbukumbu za biashara, vitabu vya hesabu na taarifa nyinginezo kama atakavyoona inafaa kufanyiwa uchunguzi kwa ajili ya kupata na/au kujua kiwango sahihi cha kodi anachotakiwa kulipa mlipa kodi husika.

Upatikanaji wa taarifa za tathmini

8.-(1) Mkurugenzi anaweza, kwa taarifa ya maandishi kumtaka mlipa kodi au wakala yeyote kuwasilisha kwake kumbukumbu za kibiashara na vitabu vya hesabu, kwa nia ya

kupata taarifa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini au kukusanya kodi ya huduma.

(2) Kwa nia ya kupata taarifa kwa mujibu wa kifungu cha 8(1) cha Sheria Ndogo hizi Mkurugenzi anaweza kumtaka mtu yeyote kufika mbele yake au kwa Afisa Muidhinishwa katika muda na mahali kadri atakavyoona inafaa.

Uwasilishaji wa hesabu

9. Kila mlipa kodi au wakala atatakiwa kutoa taarifa na au kuwasilisha hesabu za awali na kulipa kodi inayotakiwa katika muda kama ifuatavyo:-

(a) Kwa waagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi watalipa kodi katika muda itakavyokuwa imeelekezwa na Kamishna wa Kodi ya Forodha na kodi ya mlaji.

(b) Wazalishaji wa bidhaa za viwandani watalipa kodi kama itakavyoelekezwa na Kamishna wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) isipokuwa haitakuwa zaidi ya muda wa kulipa kodi ya mlaji au kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

(c) Wafanyabiashara wengine watalipa kodi katika awamu nne (04) awamu ya kwanza ikianza katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kuanza kwa kipindi cha mahesabu kwa kuzingatia mwaka wa Serikali.

Kamishna wa kodi ya forodha/ mapato.

10. Mkurugenzi anaweza kumteua Kamishna wa Kodi ya Forodha au kodi ya mapato kutathimini na kukusanya kodi ya huduma kutoka kwa mlipa kodi yeyote na kuiwasilisha kwa Halmashauri kwa wakati na muda kama itakavyoelekezwa katika kifungu cha 9 cha Sheria Ndogo hizi.

Wakala wa kukusanya kodi ya huduma

11. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi, Halmashauri inaweza kuteua wakala wa kukusanya kodi ya huduma kwa niaba yake na wakala atakayeteuliwa atakuwa na jukumu la;

(a) Kuwasilisha majumuisho kwa Mkurugenzi au Afisa Mwidhinishwa;

(b) Kuwasilisha kodi aliyokusanya katika kipindi maalum;

(c) Kuandaa na kuwasilisha kwa Halmashauri orodha ya walipa kodi ya huduma waliolipa na ambao hawajalipa kodi ya huduma katika maeneo aliyopewa uwakala.

Hesabu za mwisho

12. (1) Kila mlipa kodi au mkusanya kodi atatakiwa kuwasilisha kwa Halmashauri hesabu za mwisho katika kipindi cha miezi mitatu tangu kumalizika kwa kipindi cha hesabu ya kodi anayostahili katika mkupuo mmoja.

(2) Mlipa kodi au wakala anapowasilisha hesabu zake, Afisa Mwidhinishwa anaweza.

(a) Kupokea na kukubali kiwango cha hesabu hizo na kutathimini kodi katika msingi huo;

(b) Kukataa kupokea na badala yake kufanya tathimini kuhusu kiwango cha hesabu cha mlipa kodi huyo iwapo atakuwa na sababu za kimsingi za kuamini kuwa hesabu hizo siyo sahihi;

(3) Iwapo mlipa kodi hajawasilisha majumuisho ya hesabu zake kwa mwaka wowote wa pato na ametakiwa kufanya hivyo,Mkurugenzi au Afisa Mwidhinishwa anaweza kwa kadri atakavyoona inafaa, kuamua kiwango cha hesabu za mlipa kodi huyo,kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(4) Kodi iliyothaminiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo

hizi, italipwa katika siku thelathini tangu tarehe ya kufanya tathimini.

Makosa na Adhabu

13.(1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi mtu yeyote,kampuni au taasisi ya kibiashara atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) Atashindwa kuwasilisha hesabu sahihi na za kweli kwa Halmashauri

(b) Atazembea, kushindwa au kukataa kulipa kodi ya huduma kwa Halmashauri

(c) Atashawishi mtu mwingine kutolipa kodi anayopaswa kulipa au kumsaidia mtu mwingine kutoa taarifa za uongo kuhusu kodi anayopaswa kulipa

(d) Atakusanya kodi au kujaribu kukusanya kodi bila kibali cha Halmashauri au Afisa Mwidhinishwa

(e) Atakusanya kodi kwa kiwango ambacho hakikutajwa na sheria hii au sheria nyingine

(f) Atapotosha Halmashauri au wakala wa Halmashauri au Afisa mwidhinishwa au Kamati ya tathmini ya Halmashauri katika suala lolote linalohusu kukusanya kodi

(g) Atashindwa kuwasilisha nyaraka, maelezo au taarifa inayotakiwa kuwasilishwa kwa Halmashauri katika muda uliowekwa

(h) Atashindwa kutunza kumbukumbu yoyote au nyaraka kwa ajili ya uchunguzi

(i) Atafanya hesabu za uongo kwa kupunguza au kutoa hesabu zisizo sahihi

(j) Atatoa taarifa isiyosahihi kuhusu jambo lolote linaloweza kuathiri jukumu lake au jukumu la mtu mwingine linalohusu kulipa kodi ya huduma

(k) Ataandaa au kutengeneza au kusababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa vitabu vya uongo vya hesabu au kumbukumbu

(l) Atamzuia au atajaribu kumzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhinishwa au Wakala kutekeleza majukumu yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi

(m) Ataficha taarifa au baadhi ya taarifa ya hesabu zake kwa nia ya kupunguza kiwango cha kodi anachotakiwa kulipa

(n) Ataharibu kwa makusudi taarifa au mfumo wa taarifa za kodi kwa nia ya kupunguza au kuficha kiwango cha kodi anachotakiwa kulipa;

(o) Aliyetakiwa kutoa taarifa akazembea, kukataa au bila sababu yoyote akashindwa kutoa taarifa

(p) Atazembea, atashindwa au atakataa kuhudhuria kwa wakati na mahali palipopangwa na Halmashauri, Afisa Muidhinishwa au Kamati ya uthamini

(q) Atashindwa kwa namna yoyote kutekeleza Sheria Ndogo hizi.

(2) Mtu yeyote, Kampuni, taasisi ya kibiashara atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi kwa kufanya mambo yaliyoainishwa katika kifungu cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi Shilingi Elfu Hamsini (Tshs.50,000/=) kwa kosa lolote atakalolitenda kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 13(1) (a hadi n) na (q) pamoja na kulipa kodi ya huduma anayodaiwa au kutumikia kifungo kisichozidi miezi sita (6) jela au adhabu zote kwa pamoja yaani kifungo na faini.

(3) Mtu yeyote, Kampuni, taasisi ya kibiashara atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi kwa kufanya mambo yaliyoainishwa katika kifungu cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini

isiyozidi Shilingi Elfu Hamsini (Tshs.50,000/=) kwa kosa lolote atakalolitenda kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 13(1) (o) na (p) pamoja na kulipa kodi ya huduma anayodaiwa au kutumikia kifungo kisichozidi miezi mitatu (3) jela au adhabu zote kwa pamoja yaani kifungo na faini.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 13(2) na (3) cha Sheria Ndogo hizi mkosaji atawajibika kuilipa Halmashauri gharama zote zilizoingiwa na Halmashauri kutokana na kuvunja masharti ya Sheria Ndogo hizi

Riba itakayotozwa kwa kodi ya huduma isiyolipwa

14. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo mtu yeyote anayetakiwa kulipa kodi ya huduma atashindwa kuwasilisha hesabu zake kama inavyotakiwa katika kipindi kilichoongezwa atatozwa riba ya asilimia Ishirini (20%) kwa Mwezi.

Mamlaka ya Mkurugenzi kufifilisha kosa

15. Bila ya kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hizi Mkurugenzi atakuwa na uwezo au mamlaka ya kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi elfu Hamsini (Tshs.50,000/=) pamoja na Kodi ya huduma inaopaswa kulipwa na mhusika kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mkosaji kwa hiari yake mwenyewe atakiri kosa hilo kwa kujaza fomu maalum iliyoanishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Kufutwa kwa Tangazo la serikali No.423 la tarehe 15/10/ 2004

16. Sheria ndogo za (Service Levy, GN.423/2004) za Halmashauri ya Wilaya ya Geita za mwaka 2004 zimefutwa na Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI

Halmashauri ya Wilaya ya Geita

———

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

(*Chini ya Kifungu cha 15 cha Sheria Ndogo za (Kodi ya Huduma) za Halmashauri.*

Mimi…….....wa S.L.P…….ninayefanya biashara ya …..katika eneo la ……lililopo katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita, nakiri mbele ya .....(mkurugenzi) kwamba tarehe……mwezi……mwaka……nilikiuka kifungu cha ……..cha Sheria Ndogo za (Kodi ya Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Geita za mwaka, 2015.

Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushurutishwa na mtu yeyote nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi ataamua kutekeleza madaraka yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Jina.....

Saini.....

Mbele yangu:

Jina…….....……

Wadhifa.....

Saini.....…….....……..

Tarehe.....

.